# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 036 DISEMBA 2023

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY




1. KATIBU MKUU UCHUKUZI AAGIZA TMA KUTANGAZA MAFANIKIO KIKANDA

2. DKT. CHANG'A ATOA WITO KWA VIJANA KUSHIRIKI KIKAMILIFU KATIKA SAYANSI NA TATHMINI YA MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA TABIANCHI



3. FAHAMU ZAIDI: HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI, 2024



## KITAIFA

# KATIBU MKUU UCHUKUZI AAGIZA TMA KUTANGAZA MAFANIKIO KIKANDA

**Arusha**




Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius. W. Kahyarara alitembelea banda la maonesho la TMA katika Mkutano wa 16 wa Wadau wa Sekta ya Uchukuzi kuhusu Ufuatiliaji na Tathmini (16th JTSR) uliofanyika jijini Arusha, tarehe 05 hadi 08 Desemba 2023 na kuagiza Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kutangaza mafanikio ya taasisi yanayopatikana kikanda, kimataifa pamoja na mafanikio yanayopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Taasisi. Prof. Godius. W. Kahyarara pia ameisifu TMA kuwa ni taasisi inayofanya kazi nzuri na yenye mafanikio kitaifa na kimataifa.

Katibu Mkuu alisisitiza kuwa “ni wakati sasa, jamii ikatambua mafanikio ya TMA kikanda na kimataifa, natambua kuwa taasisi hii inafanya kazi nzuri inayoonekana, ni vyema kujipanga kuwa na vipindi katika televisheni na kueleza mafanikio hayo”. Alizungumza Prof. Godius. W. Kahyarara, wakati akitembelea mabanda ya maonesho ya wadau wa sekta ya Uchukuzi. Aidha, Prof. Godius. W. Kahyarara aliitaka Wizara kusimamia program ya kutangaza mafanikio ya Taasisi zilizo chini yaWizara ya Uchukuzi kwa kuanza na TMA.

Naye, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu TMA ambaye pia ni Mkurugenzi wa Huduma za Miundombinuna Ufundi, Dkt. Pascal Waniha, alieleza kuwa TMA imekuwa kielelezo bora katika ukanda wa Afrika Mashariki pamoja na nje ya Kanda. “Kazi kubwa imeendelea kufanyika katika kuiwakilisha nchi vizuri kwenye masuala ya hali ya hewa kimataifa na kueleza kuwa imeteuliwa na WMO kuwa muandaaji wa mafunzo ya rada katika Kanda ya Afrika yanayoratibiwa na Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO). Fursa hii imepatikana kutokana na uwekezaji mkubwa wa miundombinu ya hali ya hewa unaoendelea kufanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania”. Alisema Dkt. Waniha.

Mafanikio mengine yaliyoelezwa mbele ya Katibu Mkuu kupitia mabango ni pamoja na maendeleo katika shughuli za uangazi, ununuzi wa vifaa na mitambo ya hali ya hewa, udhibiti wa huduma za hali ya hewa pamoja na njia mbalimbali zinazotumika katika kusambaza taarifa za hali ya hewa kwa jamii na kwa sekta mahsusi.



## KIMATAIFA

# DKT. CHANG'A ATOA WITO KWA VIJANA KUSHIRIKI KIKAMILIFU KATIKA SAYANSI NA TATHMINI YA MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA TABIANCHI

**Dubai, UAE**



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi "Intergovernmental Panel on Climate Change (IPCC)", Dkt. Ladislaus Chang'a, alitoa wito wa kuimarisha ushiriki wa vijana katika sayansi ya mabadiliko ya hali ya hewa na shughuli za Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi (IPCC).

Dkt. Chang'a alitoa wito huo tarehe 8 Desemba, 2023 kwenye Mkutano wa 28 wa Umoja wa Mataifa wa mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi "United Nations Climate Change Convention Conference of Parties (UNFCCC COP28) ", uliofanyia Jijini Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu kuanzia tarehe 30 Novemba hadi 12 Desemba, 2023. Alitoa wito huo alipoongoza mjadala kuhusiana na "Mabadiliko katika Mfumo wa elimu kuwajengea uwezo vijana, na Uimarishaji wa ushiriki wa vijana katika sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na shughuli za Jopo la IPCC **(Transforming**

**education to empower youth and enhancing the participation of young people in climate change science and IPCC process: challenges, opportunities, lessons learned)".** Mjadala huo uliandaliwa na jopo la IPCC kwa kushirikiana na kampuni za "Philanthropy Cortes Solari" na "MERI Foundation".




Akifungua mjadala huo, Dkt. Chang'a alitaja na kufafanua vipaumbele vya IPCC katika Mzunguko wa Saba wa Tathmini ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi "Seventh IPCC Assessment Cycle (AR7). Kipaumbele kimojawapo alichoainisha ni kuimarisha ushiriki wa vijana katika mchakato mzima wa Tathmini ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi Duniani.

*"Kipaumbele hiki cha IPCC kinalenga kuimarisha ushiriki wa vijana, sio tu katika upatikanaji wa taarifa za mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi, bali katika mchakato mzima wa tathmini yenyewe na ikiwa ni pamoja usambazaji wa taarifa ya tathmini".* Alisema Dkt. Chang'a. Aidha alifafanua kuwa mjadala huo ulijielekeza zaidi kujadili changamoto, fursa, mambo ya kujifunza na faida zinazotokana na ushiriki wa vijana katika sayansi ya mabadiliko ya hali ya hewa na shghuli za IPCC, kwa lengo la kukuza ushiriki wa vijana katika sayansi ya mabadiliko ya hali ya hewa na shughuli za IPCC, hususan wakati wa Tathmini ya Saba ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi.

Mjadala huo ulihusisha mada mbalimbali zilizohusiana na lengo la mjadala huo. Miongoni mwa waliowasilisha mada ni baadhi ya viongozi wa Jopo la IPCC wa sasa na waliomaliza muda wao, mwakilishi kutoka Sekretarieti ya IPCC, maafisa viungo wa nchi katika Jopo la IPCC (IPCC Focal Points), na wawakilishi kutoka mashirika yanayojihusisha na vijana na watoto, ikiwa ni pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na watoto la UNICEF.

Mada zilizowasilishwa ni pamoja na: Fursa zinazotolewa na IPCC kwa vijana ikiwa ni pamoja na Programu ya Ufadhili kwa wanafunzi wanaofanya utafiti kuhusiana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na faida za ufadhili huu. Aidha watoa mada wengine walijikita katika kuainisha changamoto za ushiriki mdogo wa vijana na mikakati ya kukabiliana na hizo changamoto ili kuimarisha ushiriki wa vijana. Hii ilijumuisha watoa mada walioainisha uzoefu kutoka Mabara ya Afrika na Ulaya na nchi mbalimbali kama vile Japan, Ghana na Kenya. Aidha, washiriki wa mjadala huo walitoa michango na ushuhuda wa namna wanavyohusisha vijana katika masuala ya kukabiliana namabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na kuuliza maswali mbalimbali ambayo yalitolewa ufafanuzi.

Akihitimisha mjadala huo, Dkt. Chang'a alisisitiza kwamba licha ya changamoto zilizotolewa, uimarishaji wa ushiriki wa vijana katika masuala ya sayansi ya mabadiliko ya hali ya hewa na shughuli za IPCC, inawezekana na ni muhimu kuhakikisha vijana wanachangia ipasavyo katika

kutatua changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi Duniani.

*"Uimarishaji wa ushiriki wa vijana katika masuala ya sayansi ya mabadiliko ya hali ya hewa na shughuli za IPCC ni muhimu sana na tumejipanga kufanya hivyo katika miaka saba ijayo".* Alisema Dkt. Chang'a na kuwahakikishia washiriki kuwa mawazo yote yaliyotolewa yatazingatiwa na IPCC katika kufanya maboresho stahiki. Pia aliwashukuru washiriki kwa michango mbalimbali waliyotoa katika mjadala huo.

Sanjari na mjadala huo, Dkt. Chang'a alishiriki pia katika vikao mbalimbali vilivyohusu mchango wa vijana na watoto katika mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi, ambapo aliendelea kuwasisitiza vijana na watoto kuwa chachu ya mabadiliko kwa kushiriki katika sayansi ya mabadiliko ya hali ya hewa na shughuli za IPCC. *"Vijana na watoto ni mawakala wazuri sana wa mabadiliko na kwa hivyo wana jukumu muhimu sana katika kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi",* Alisema Dkt. Chang'a. Miongoni mwa vikao alivyoshiriki ni Mdahalo wa Vijana na Watoto kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi (Youth and Children Climate Change Dialogue) ulioandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la UNICEF tarehe 8 Desemba, 2023 kujadili athari za mabadliko ya hali ya hewa na tabianchi kwa watoto na vijana.

Katika hatua nyingine, Dkt. Chang'a alialikwa kuwa miongoni mwa wazungumzaji (Panelist) katika mjadala ulioandaliwa na Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) kuhusiana na faida za huduma za hali ya hewa katika shughuli za kiuchumi (Socio-economic benefits of weather and climate services) uliofanyika tarehe 8 Desemba, 2023. Vilevile alishiriki katika mkutano ulioandaliwa na viongozi wa IPCC uliohusu uwasilishaji wa taarifa ya Tathmini ya Sita ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi na kuainisha mapungufu ya kushughulikiwa katika tathmini ya saba. Aidha, Dkt. Chang'a alifanya kikao na Ujumbe wa Wizara ya Elimu, Utamaduni, Michezo, Sayansi na Teknolojia ya Japan na kujadili masuala ya ushirikiano katika kujenga uwezo wa wataalamu katika masuala ya hali ya hewa na mchango katika mfuko wa ufadhili wa wataalamu wa IPCC.

Ikumbukwe kwamba Mkutano wa COP28 hufanyika sambamba na mikutano ya pembezoni (side events) na mikutano ya uwili (bilateral meetings). Katika mkutano wa COP 28, Dkt. Chang'a akiwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA alikuwa sehemu ya Ujumbe wa Tanzania ambapo ushiriki wa TMA katika mkutano huo ulikuwa fursa ya kutoa mchango wa kitaalam kuhusu sayansi ya mabadiliko ya hali ya hewa katika majadiliano na maamuzi ya COP28 kwa manufaa mapana ya nchi yetu. Aidha, Dkt. Chang'a akiwa Mwakilishi wa kudumu wa Tanzania katika WMO na Makamu Mwenyekiti wa Jopo la IPCC, alishiriki katika programu na vikao vilivyoandaliwa na WMO na IPCC sambamba na mkutano huo wa COP28. Pamoja na majukumu mengine katika uongozi wa jopo la IPCC, Dkt.Chang'a amepewa na IPCC jukumu maalumu la kuratibu na kuhamasisha vijana duniani kote kushiriki na kutoa mchango katika Sayansi ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na namna ya kukabiliana na mabadiliko hayo na kushiriki katika shughuli za IPCC, jukumu ambalo alilitekeleza kwa ufanisi wakati wa Mkutano wa COP28.



TMA
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

# FAHAMU ZAIDI

## HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI, 2024

Mvua zinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka. Kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, mvua za nje ya msimu zinatarajiwa katika kipindi cha mwezi Januari, 2024. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini. Kwa upande mwingine, hali ya joto inatarajiwa kuendelea husisan katika baadhi ya maeneo yanayotarajiwa kupata vipindi vichache vya mvua.

| MAENEO | MAELEZO |
|---|---|
| Pwani ya Kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba): | ♦ Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika maeneo machache, hususan katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.** |
| Nyanda za juu Kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): | ♦ Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa kati wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.** |
| Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): | ♦ Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Ongezeko la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza ya mwezi.** |
| Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): | ♦ Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha ongezeko la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili.** |
| Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): | ♦ Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache, hususan katika wiki ya kwanza ya mwezi.** |
| Nyanda za juu Kusini Magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro): | ♦ Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo kwa vinatarajiwa katika maeneo mengi. **Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili.** |
| Pwani ya Kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): | ♦ Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo vinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa, hususan wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.** |
| Kanda ya Kusini (Mkoa wa Ruvuma): | ♦ Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.** |

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

# BIDHAA NA HUDUMA ZA TMA

## HUDUMA ZA HALI YA HEWA KWA SEKTA YA MAZINGIRA

Mamlaka ya Hali ya hewa Tanzania (TMA) inatoa huduma za hali ya hewa zinazosaidia sekta ya Mazingira katika kudhibiti athari zinazohusiana na hali mbaya ya hewa. Huduma hizi zinatolewa kwa kufuata na kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Mamlaka hutoa huduma zifuatazo za hali ya hewa kwa shughuli za mazingira; -**

(a) Taarifa za jumla za hali ya hewa.
(b) Takwimu na taarifa za ongezeko la joto duniani na mabadiliko ya tabianchi.
(c) Takwimu za uchafuzi wa angahewa.
(d) Takwimu za klimatolojia kama ilivyoanishwa kwa eneo maalum ikiwemo matukio ya hali ya hewa yaliyokithiri.
(e) Utabiri wa hali ya hewa mahsusi (maalum) na tahadhari za matukio ya hali mbaya ya hewa.
(f) Kasi na mwelekeo wa upepo
(g) Ripoti za Tsunami
(h) Huduma nyingine zozote zinazohusiana.

**Wateja wa sekta ya mazingira hutumia huduma za hali ya hewa kwa shughuli zifuatazo za mazingira-**

(a) Kuweka msingi katika kupanga kwa ajili ya kupunguza upotevu wa mali na mali asilia na za kimazingira pamoja na masuala mengine ikiwemo kujua maeneo ya bahari ambayo umwagikaji wa mafuta unaweza kujitokeza na kufika katika mwambao.
(b) Uhifadhi wa mabaki yanayotokana na bidhaa zinazozalishwa au zinazotengenezwa kutoka viwandani kama vile mbolea na saruji pamoja na vitu vingine.
(c) Kupunguza uchafuzi wa mazingira.
(d) Tathmini ya athari na mkakati/mpango/sera katika kufanya tathmini kwa Mazingira.
(e) Udhibiti wa taka.
(f) Shughuli nyingine yoyote inayohusiana.






JARIDA LA MWEZI
TOLEO NA. 035
NOVEMBA 2023
TMA
1 TMA NA SHIRIKA LA MSALABA MWEKUNDU TANZANIA WASAINI MAKUBALIANO YA MASHIRIKIANO YA UTOAJI ELIMU NA USAMBAZAJI WA TAARIFA ZA HALI YA HEWA
2 DKT. CHANG'A APEWA JUKUMU LA KUSIMAMIA BODI YA SAYANSI KATIKA JOPO LA KIMATAIFA LA SAYANSI YA MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA TABIANCHI (IPCC)
3 FAHAMU ZAIDI: HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI NOVEMBA, 2023
ISO 9001: 2015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga

**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**


**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Monica Mutoni
Wilbert Muruke

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Kituo Kikuu cha Utabiri
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa



www.meteo.go.tz

@tmaservices

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

TMAonline TV

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu,
1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27,
41218 DODOMA.